# USAWIRI CHANYA WA WATOTO KATIKA FASIHI YA WATOTO KAMA NJIA FAAFU YA KUJENGA JAMII BORA YA LEO NA KESHO: MIFANO KUTOKA VITABU TEULE VYA WATOTO VYA KISWAHILI

*Leonard H. Bakize*

**Ikisiri**

*Mshengyezi (2003) anadai kuwa, fasihi siyo tu matokeo ya matendo ya wanajamii, bali pia, ni wakala mzuri wa kuipa jamii mwelekeo mzuri kama ikisawiri mambo vizuri na ikatumiwa vizuri. Memmi (2006) anasisitiza kuwa waandishi wa fasihi wana chombo muhimu sana mikononi mwao ambacho kutokana na ubunifu wao, huwawezesha wasomaji kuamini na kuathirika kutokana na kile wanachokisoma au kusikiliza. Memmi (keshatajwa) anaongeza kuwa hata kama kazi fulani ya fasihi ni ya kubuni, bado wahusika wake wanaweza kubebeshwa mawazo ya waandishi kuhusiana na jinsi ambavyo wasanii huyaona maisha na jinsi wanavyotamani maisha hayo yawe. Hivyo, yeye anahitimisha kwa kusema kuwa, fasihi ni chanzo muhimu sana cha ujenzi wa taifa endelevu. Lengo huu la makala hii ni kushadidia hoja kwamba, fasihi ya watoto ikiwasawiri vyema watoto na kuwaonesha kuwa ni watu muhimu, tunaweza kuwa na jamii bora leo na kesho. Makala inachambua na kubainisha hoja zake kwa kutumia kazi kumi na moja za Kiswahili zilizoandikwa kwa ajili ya kusomwa na watoto. Makala inaongozwa na Nadharia za Usimulizi na Kisosholojia. Katika matokeo ya uchambuzi wa data, inabainika kwa uwazi kwamba, watoto wanaposoma, huamini yale wanayoyasoma; hivyo kuwa na uwezekano mkubwa wa kubadilishwa na kile wanachokisoma. Hivyo, kama tukichukua tahadhari tukawasawiri vyema watoto, kama asemavyo Memmi (2006), tunayo nafasi kubwa ya kuwaathiri vizuri watoto ili wajenge jamii nzuri.*

## Utangulizi

Utafiti mdogo uliofanywa na Matundura, Kobia & Mukuthuria (2014) kuhusu masuala ya uana ulionesha kwamba baadhi ya waandishi wanaendeleza taswira dumifu za uana zinazoendeleza ubaguzi wa kijinsia. Katika matini walizochambua walibaini kwamba waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wanamsawiri mhusika wa kike kama kiumbe dhaifu, mtulivu, mlezi, na mtegemezi wa mwenzake wa kiume, huku mhusika wa kiume akisawiriwa kama mwenye nguvu, mwenye kuthubutu, na uwezo mkubwa wa kufanya mambo. Pia, walibaini kwamba mhusika wa jinsi ya kike anabaguliwa katika masuala ya urithi wa mali, hasa ardhi, na kunyimwa haki ya kwenda shuleni. Ingawa makala hii haipingi matokeo ya utafiti

huo, inataka kuonesha upande wa pili wa shilingi kwamba wahusika hao wa kike na kiume wanaposawiriwa kwa kuendeleza mawazo mgando ya kijamii, huenda ikawa ni kuwapoteza zaidi watoto wanaosoma vitabu hivyo. Hii ni kwa sababu kutokana na kiwango kidogo cha kufikiri, basi watoto wengi huamini mambo mengi wanayoyasikiliza katika hadithi na pale wanaposoma vitabu tunavyowapa wasome. Fikra hii inashadidia hoja za tafiti nyingine zilizowahi kufanyika zikiwa na mwelekeo karibu sawa na wa makala hii (taz. Weche, 2002; Ruthiiri, 2012 & Ngugi, 2014). Usawiri unaoendeleza mawazo mgando huenda ukaendeleza mawazo hayo badala ya kuachana nayo. Makala inaangalia usawiri wa mtoto katika mtazamo chanya kwa jumla na jinsi usawiri huo unavyoweza kujenga jamii yenye mwelekeo mzuri zaidi.

## Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Utafiti uliozaa makala hii ulikuwa wa maktabani. Data zilipatikana kwa njia ya usomaji wa vitabu vya watoto kumi na moja. Navyo ni: *Vijana Jasiri* (Shija, 1980), *Ngome ya Mianzi* (Mulokozi, 1990), *Tanzua* (Mwandoloma, 1991), *Bahati na Mumewe* (Mwenda, 1995), *Safari ya Muzimuni* (Mateso, 2005), *Kimbia Helena Kimbia* (Mnyaka, 2005), *Yatima* (Wamitila, 2006), *Wema na Albino* (Mkufya, 2008), *Vipaji vya Helena* (Mnyaka, 2009), *Kijana Hodari* (Porini, 2011) na *Usiku wa Balaa* (Dumea, 2012). Uteuzi wa vitabu hivyo ulizingatia, kwa kiasi fulani, kigezo cha kuandikwa na wanawake na wanaume ijapokuwa si kwa ulinganifu wa idadi. Pia, tumechagua vitabu kwa kuchanganya vilivyochapishwa Kenya na Tanzania, ijapokuwa ulinganifu wa idadi haukuzingatiwa. Hata hivyo, kigezo kikuu cha uteuzi huo kilikuwa maudhui yanayopatikana kutokana na usawiri wa wahusika. Tuliangalia vitabu ambavyo vimemsawiri mtoto katika hali chanya ili kuwezesha ushadidizi wa hoja zetu. Hatukuzingatia kigezo cha kuchanganya tanzu za uandishi, yaani riwaya, tamthilia, utenzi na fasihi simulizi. Kutokana na historia ya uchapishaji wa vitabu vingi vya watoto Kenya na Tanzania, vitabu vingi vinatokana na fasihi simulizi. Hivyo, kazi zinazopatikana zaidi ni riwaya fupi na hadithi fupi. Nasi tumezichukua hizo kwa kuwa zinapatikana kirahisi na ndizo zinazosomwa zaidi na watoto husika shuleni.

## Mwega wa Kinadharia

Makala hii inaongozwa na mawazo ya nadharia za Usimulizi/Naratolojia na Kisosholojia. "Naratolojia ni nadharia inayojihusisha na usimulizi unaopatikana katika matini ambayo yaweza kuwa ya mdomo, iliyochorwa au iliyoandikwa" (Ilomo, 2012:18). Bal (1997) anadai kuwa Naratolojia ni nadharia inayohusu matini simulizi, vichekesho, matukio, na vyombo vya kiutamaduni, ambavyo vyote ni hadithi ya kusimulia. Wamitila (2002), akimnukuu Prince (1987), anafafanua usimulizi kama uelezaji wa tukio moja au mengi ya kihalisi au ya kibunilizi… tokeo na njia, lengo na tendo, muundo na uundaji (wake). Ilomo (2012) anafafanua kuwa wataalamu wa nadharia hii wanaelekea kukubaliana kuwa msingi mkuu wa

nadharia hii ya usimulizi ni msimulizi mwenyewe. De Jong (2004) anaona kuwa, msimulizi ni muhimu katika nadharia hii kwa sababu kuwapo kwa msimulizi ndicho kigezo kikuu cha matini kuwa simulizi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), Naratolojia ni nadharia ambayo imetokana na dhana ya Kifaransa *narratologie* iliyoanzishwa na Tzvetan Todorov katika kitabu chake kiitwacho *Grammaire du Decameron* (1969). Ilomo (2012:18-19) anafafanua kuwa "msingi mkuu wa nadharia hii ni kuzichunguza na kuzichanganua sifa za usimulizi ili kubainisha mfumo maalumu wa kanuni zinazohusika kuvyaza simulizi pamoja na ukuaji wake." Msingi huu unaihusisha nadharia hii na mkondo wa jadi wa Umuundo wa Kifaransa (Wamitila, 2002). Hata hivyo, inaelezwa kuwa nadharia hii ya Naratolojia iliwekewa misingi yake na mawazo ya mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato, katika andiko lake liitwalo *Republic III.* Wamitila (keshatajwa) anaeleza kuwa, mawazo ya Plato yanafumbatwa na dhana mbili: *mimesia* na *daigesia.* Katika *mimesia*, mtunzi hajitokezi wazi kama msemaji, ilhali katika *daigesia* msimulizi hujitokeza waziwazi, hivyo anaweza kutambulika. Kwa hiyo, kupitia usimuliaji, msimulizi anajenga mkabala ambao unamwezesha msomaji au mtazamaji kuyatazama yanayotendeka na kuyasikia yanayosimuliwa (Burundi, Mukuthuria na Matundura, 2014).

Nadharia hii inahusika na uchunguzi wa hali, muundo na uamilifu wa hadithi na kubainisha umilisi wa kisimulizi alionao mtunzi. Aidha, huchunguza sifa zinazohusisha simulizi na kuzitenganisha na nyingine (Burundi na wenzake, weshatajwa). Msimulizi au mwandishi wa hadithi huwa na mtazamo kuhusu masuala kadhaa ambayo hutaka kushirikisha hadhira. Hali ya msimulizi au mwandishi kutaka msomaji wake aone na kutazama mambo kama mwandishi atakavyo huitwa utazamishaji (*focalization*). Makala hii inajikita katika dhana hiyo kwa maana ya kwamba, vitabu tutakavyovichambua, waandishi wake wanawatazamisha watoto kuelewa kwamba wana nafasi kubwa ya kuibadilisha jamii kwa nafasi zao mbalimbali walizonazo.

Nadharia ya pili inayoongoza makala hii, nadharia ya Kisosholojia, inadai kuwa kazi mbalimbali za kifasihi zinatokana na matukio ya kijamii. Hivyo, jamii ndiyo malighafi ya kazi za fasihi. Lakini kwa upande wa pili, kazi za fasihi zina nafasi kubwa katika kuathiri jamii vizuri au vibaya. Hii inaonesha kuwa msanii ni wakala wa mabadiliko ya jamii kupitia kazi zake za kifasihi. Baada ya kazi za msanii kukamilika, huwafikia wasomaji/wasikilizaji ambao ndio walengwa wa kazi hiyo. Matokeo ya kazi ya msanii wa fasihi kusomwa/kusikilizwa ni kuipa jamii mustakabali mzuri au mbaya (Bakize, 2013). Katika jamii, watu husema kuwa taifa lisilo na watoto ni taifa lisilo na uhai endelevu. Hii humaanisha kuwa watoto ni watu wazima wa kesho. Kama watoto wakiandaliwa vizuri leo, maana yake ni kwamba tunaweza kuwa na jamii nzuri kesho

au kinyume chake. Ukweli huo unajengwa na mawazo makuu ya nadharia ya Sosholojia katika fasihi ambayo hudai kuwa fasihi ni chombo cha kuleta mabadiliko kijamii; siyo tu kwa ajili ya kuleta burudani bali kufundisha, kukanya na kuipa jamii mustakabali mzuri (Mshengyezi, 2003). Fasihi siyo tu matokeo ya matendo ya wanajamii, bali pia, ni wakala mzuri wa kuipa jamii mwelekeo mzuri kama ikitumiwa vizuri. Mawazo ya nadharia hii yanaisaidia makala hii katika kutabiri matokeo ya athari ya usomaji wa kazi za watoto.

Hivyo basi, ni matarajio yetu kwamba kwa mtazamo wa nadharia hii, kazi teule zinaposomwa na watoto huwabadilisha na kuwa watu wengine. Kwa kuwa watoto huamini kile wanachokisoma (Weche, 2002; Ruthiiri, 2012; & Ngugi, 2014), basi endapo wamesawiriwa vizuri kama vyombo vya kuleta mabadiliko katika jamii, huenda jamii zetu zikabadilika kwa sababu ya usawiri huo mzuri. Makala inakazia kuwa, watoto hupenda kuiga mambo mazuri wanayoyasoma katika kazi za fasihi. Hivyo, kama kazi zinaonesha wahusika watoto wakiwa katika harakati za kuleta mabadiliko, si ajabu na wasomaji wa vitabu hivyo nao wakajifunza na kuweka matendoni yale waliyoyasoma.

**Uchambuzi wa Vitabu Teule**

Baada ya kufanya usomaji wa kina wa vitabu teule, tumefanya uchambuzi ambao umejikita katika maudhui zaidi. Tumeangalia jinsi mtoto, hasa mhusika au wahusika wakuu, walivyochorwa katika kazi hizo. Uchambuzi wetu, kama tulivyodokeza hapo awali, umeongozwa na viunzi viwili vya nadharia, yaani Nadharia ya Usimulizi na Nadharia ya Kisosholojia. Baada ya kusoma vitabu hivyo teule na kuongozwa na mawazo ya nadharia tulizoziteua, tumebaini kuwa, watoto wamechorwa katika namna chanya mbalimbali kama zitakavyobainishwa na kudadavuliwa katika vipengele vitakavyofuata.

**Kusawiriwa Vizuri katika Mahusiano ya Kijinsia**

Usawa wa kijinsia ni suala mojawapo katika mambo yanayopigiwa upatu duniani leo. Tofauti za kijinsia bado zinajitokeza katika jamii mbalimbali katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Kutokana na mitazamo potofu ya kijamii na mifumo ya maisha, wanaume wanapewa nafasi za kwanza katika mambo mengi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa (Matundura na wenzake, 2013). Hivi sasa tunaona juhudi za serikali za nchi nyingi zikipambana na hali hii ili kuwapa wanawake nafasi muhimu katika kuweka usawa wa kijinsia. Katika kazi za fasihi, mwachano wa kijinsia unaoneshwa kama suala la kimapinduzi. Ni katika mtazamo huu, tunamuona Nyawelu (msichana) akishikilia nafasi sawa na Mugoha (mvulana) katika kupigana vita vya Wahehe dhidi ya Wadachi. Mulokozi anaweka wazi katika *Ngome ya Mianzi* kuwa, jamii zetu zinaweka tofauti za fursa kutokana na jinsi kuanzia utotoni kwa kuwaaminisha wavulana kuwa ni muhimu kuliko wasichana. Katika ukurasa wa 17, mwandishi anasema, “*Msichana mdogo*

*hivyo-utawezaje kazi hiyo ya kiume*?" Wanawake wanapewa kazi za chini katika jamii. Kazi kama za kupika, kufua nguo, kulea watoto, kuridhisha wanaume, na kuchukua masomo ya sayansi za jamii katika masomo ya sekondari kwa kuwa yanayoonekana kuwafaa. Wanaume wanapewa nafasi muhimu kama vile kuchukua nafasi nzuri za madaraka katika uongozi, kushikilia uchumi wa familia, na kumiliki mali.

Kazi za fasihi zinapaswa kurudisha usawa wa kijinsia katika fursa na kuondoa imani potofu katika jamii dhidi ya uwezo wa wanawake. Watoto wakisawiriwa vyema kifasihi katika hili, kuna uwezekano wa kuwa na jamii yenye usawa wa kijinsia hapo baadaye. Matarajio hayo ya usawa ndiyo yaliyomsukuma Mulokozi katika *Ngome ya Mianzi* akamchora Nyawelu na Mugoha kama wahusika wanaoleta mabadiliko kwa ulinganifu. Katika *Safari ya Muzimuni*, tunamuona Sara akiwa ndiye mwenye kuanzisha wazo la kuleta ukombozi wa nchi ya Wasifwe. Anashikamana na Chidi na wanapitia nyakati ngumu sana; hatimaye, kwa pamoja, wanaleta ukombozi kwa nchi yao. Msichana, Wema ambaye ni binti katika *Wema na Albino* tunamuona akisimama kidete kufanya utafiti kuhusu albino na hatimaye kuielimisha jamii nzima. Sina-Kitu, katika *Bahati na Mumewe*, anafanya uchunguzi kuhusu shemeji yake ambaye alikuwa Zimwi na hatimaye kufanikiwa kumkomboa dada yake ambaye alikuwa hatarini kuliwa na mazimwi. Katika *Kimbia! Helena, Kimbia!* Tunamuona Helena ambaye ni msichana mdogo akipambana na mazingira magumu na ya hatari kama kushinda njaa, kukimbia risasi na mabomu, kuugua kwa sababu ya uchovu na mengine kadha wa kadha, hatimaye anashinda na anakuwa shujaa. Katika *Yatima*, tunakutana na Katiwa ambaye ni yatima anavumilia na kupambana na mazingira magumu ya kuteswa, kuonewa, kusingiziwa na hatimaye kushinda. Pia, katika *Usiku wa Balaa*, tunamuona Bure akiibuka kuwa shujaa baada ya kubaki mwenyewe katika kijiji na kupambana na madhila ya kila aina.

Kuinuliwa huku kwa mashujaa wa kike kumetokana na dunia inayotamaniwa na waandishi kufikiwa. Waandishi wote wanatamani kuona kuwa msichana na mvulana wanaweza kusimama na kuleta mabadiliko bila ubaguzi wa kijinsia.

**Kuwaepusha Watoto na Imani Potofu za Kijamii**

Imani potofu kama vile za kishirikina na imani potofu dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi zinatesa jamii nyingi za Kiafrika. Watu wengi wanaamini kuwa viungo vya maalbino ni chambo kizuri cha madini huko migodini, kuwa albino hawafi bali hutoweka tu, pia watu huamini katika uchawi, hasa pale wanapougua ugonjwa usiojulikana. Kama imani hizi mbaya hazimulikwi na kukomeshwa kupitia kazi za fasihi, hatuwezi kuwa na jamii zilizoelimika hapo baadaye. Katika *Wema na Albino*, Luka anadai kuwa aliambiwa na kaka yake kwamba, viungo vya albino vinawindwa kwa ajili ya kupata madini migodini. Alidai kuwa, macho yao yanaweza kuona almasi

na sarafu za fedha zilizofichwa na Wazungu katika mashimo (uk. 2). Imani hizi ndizo zinamsukuma Wema kufanya urafiki na Noa ambaye ni albino ili apate uhakika wa mambo yasemwayo. Hatimaye, katika matokeo ya utafiti wake, Wema anabaini kuwa aliyoambiwa yalikuwa tofauti sana na ukweli wenyewe. Alibaini kuwa watoto wenye ulemavu wa ngozi (albino) ni binadamu kama wengine, isipokuwa tu, wana upungufu wa melanini katika ngozi zao. Katika *Vijana Jasiri*, watoto waliokuwa wamekwenda katika kijiji cha Mji-Mwema kwa ajili ya safari ya kimasomo, baada ya kusikia uvumi kuwa vichaka jirani vina mizimu ya watumwa, wanaanza kufanya utafiti ili kujionea ukweli. Hatimaye, watoto wanaisaidia sana jamii ya watu wa Mji-Mwema kupata suluhisho la wizi wa mali ya kijiji. Watoto wanaisaidia jamii kujua ukweli kuwa kumbe vichaka vile vilikuwa vinatumika kuficha mali za kijiji zilizoibwa. Udadisi wa watoto katika muktadha huu unabadili maisha ya wanajamii. Wanajamii wa Mji-Mwema, baada ya kubaini ukweli, hawakuibiwa tena mali zao. Hizi zilikuwa juhudi zilizofanywa na watoto katika kuipa jamii mwelekeo mpya. Pia, katika *Tanzua*, tunamuona Gwake ambaye naye anaamua kujipa kazi ya utafiti kuhusu ukweli wa imani za kishirikina ili aibadilishe jamii yake. Baada ya kukatazwa na mama yake kuwa asishirikiane na Bi Ndosi, Gwake anaamua kushirikiana naye kisirisiri ili apate uhakika wa uvumi uliokuwa umeenea katika kijiji kizima kuwa Ndosi ni mchawi. Matokeo yake, anafanikiwa kuionesha jamii kuwa kumbe Bi Ndosi hakuwa mchawi bali alikuwa akisingiziwa tu.

**Kulea Vipaji vya Watoto**

Baadhi ya watoto wana vipaji vilivyofichika. Vipaji hivyo lazima vitunzwe na kulelewa na wazazi pamoja na wote wanaohusika katika suala la malezi. Kazi za kifasihi zinapaswa kuonesha wazi kuwa baadhi ya vipaji vya watoto vimefichika na hivyo bila kuwapa watoto nafasi ya kulea vipaji vyao, hawawezi kuvionesha. Kamau, katika *Kijana Hodari*, ni miongoni mwa watoto wenye vipaji vilivyofichika. Porini (2011) anamsawiri Kamau kama mtoto aliyewakatisha tamaa wazazi, marafiki na walimu wake kutokana na udhaifu wake katika kuonesha vipaji vyake. Hakuna aliyekuwa na tumaini dhidi yake kwani kila alichokifanya, kilikuwa kinakatisha tamaa. Ijapokuwa Kamau alijua kuwa kila mtu alikuwa amekata tamaa juu yake, yeye aliendelea kujaribu karibia kila kitu. Kwa mfano, alijaribu kucheza mpira, kuimba, na kuchora. Baada ya kujaribu vipaji kadhaa kwa muda mrefu, Kamau anaibuka na kipaji cha uchoraji. Kipaji hiki kinambadilisha jina la utani la Kamau Hawezi na kuwa Kijana Hodari. Hali hii ilitokana na juhudi binafsi za Kamau na hamasa iliyotoka kwa baadhi ya rafiki zake kama Mary, Salu na Isaya. Watoto wanapaswa kusawiriwa katika fasihi kama watu wenye vipaji ambavyo vitaipa jamii mustakabali mzuri. "*Kama utafanikiwa kuutumia usanii kurekebisha jamii utasifiwa." Isaya alisema* (uk.35). Mwandishi anasema, "*Tumpe nafasi Kamau," Salu alisema*. "*Kuna vipaji ambavyo havionekani.*

*Huenda Kamau akawa mwimbaji mzuri. Baadhi ya vipaji vimefichika," Salu alisema*, (uk. 9).

Katika *Vipaji vya Helena*, tunamuona msichana Helena anavyokuwa maarufu huko London Uingereza baada ya kuwezeshwa kimazingira. Akiwa katika madhila ya vita huko Rwanda na Kongo, hakuna mtu ambaye angeweza kubaini vipaji vyake hivyo vya ajabu. Kumbe picha tuipatayo ni kwamba mazingira faafu ni muhimu sana katika kuibua na kujenga vipaji vya watoto. Hii inaonesha kuwa watoto wanapaswa kutiwa hamasa na matumaini kupitia fasihi ya watoto ili waweze kuelewa taratibu vipaji vyao. Hii itasaidia jamii kupata watu wengi wenye vipaji vikubwa katika kucheza mipira, uimbaji, mieleka, kuogelea, ushairi, uandishi, na kadhalika.

**Kusawiri Watoto kama Wazalendo wa Nchi Zao**

Baadhi ya kazi za fasihi ya watoto hujaribu kupandikiza moyo wa utaifa na uzalendo kwa watoto wasomaji. Katika *Ngome ya Mianzi*, Mulokozi anaonesha kuwa si watu wazima tu wanaopaswa kupigania mataifa yao, bali pia watoto wanapaswa kuandaliwa kwa ajili ya kuchukua jukumu hilo pale inapobidi. Mugoha na Nyawelu wamewekwa katika nafasi ya kupigania taifa lao kutokana na uvamizi unaofanywa na Wadachi. Hapa ieleweke kuwa kinachosisitizwa si kuwahusisha watoto katika vita kama ilivyotokea huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda, Somalia au Sudani, bali kazi za fasihi ya watoto zinapaswa kuwasawiri watoto kama wazalendo wa nchi zao na walio tayari kuzilinda kwa gharama yoyote. Hali tunayoisisitiza katika makala hii ni kama ile iliyojitokeza kwa Sara na Chidi katika *Safari ya Muzimuni*. Bila hofu yoyote, vijana hao wawili waliamua kujitoa mhanga kwa ajili ya nchi yao. Kutokana na ujasiri wao, nchi ya Wasifwe iliokoka. Katika *Vijana Jasiri*, tunawaona vijana Benedikta, Mussa, Selemani, Mwanaisha, Kadudu, Amina na Mapunda Mdogo wakijitosa katika utafiti hatari wa kubaini wezi wa mali za kijiji. Katika ujasiri wao huo, wanafanikiwa kupata ukweli na kuwasaidia wakazi wa Bagamoyo kujua kuwa kumbe walikuwa wanaibiwa kila siku kwa sababu tu ya utapeli na uongo. Kwa mfano huo, waandishi wanapaswa kuandika kazi za fasihi ya watoto ambazo zinachochea ubunifu na moyo wa utafiti katika mambo mengi ili kujenga taifa bora zaidi.

**Kusawiri Watoto kama Watu Wenye UJasiri**

Kazi za fasihi zijaribu kusawiri watoto kama watu wenye ujasiri. Ujasiri unaweza kuwasaidia watoto kujenga uzalendo. "*Kuogopa si vibaya; ndio ubinadamu. Binadamu asiyeogopa mwogope… Lililo la muhimu ni kuwa tayari wakati wowote kukikabili kile unachokiogopa pale inapobidi*" (*Ngome ya Mianzi*, uk. 11). Katika maisha ya kijamii, kuna matatizo na changamoto nyingi. Watoto wanapaswa kusawiriwa katika hali ambayo inawasaidia kukabiliana na mazingira hayo kwa ujasiri. Kazi za kifasihi zina mchango mkubwa katika jukumu hili. Katika dondoo la hapo juu, Bibi anajaribu

kuwapa ujasiri Mugoha na Nyawelu kwamba japo wana woga, wanapaswa kuushinda na kusimama imara katika mazingira ya hatari.

Katika *Safari ya Muzimuni*, Sara na Chidi wamechorwa kama majasiri walioiletea ukombozi nchi ya Wasifwe. Katika *Tanzua*, Gwake anaamua kujiingiza katika mazingira hatarishi na magumu ili tu aweze kupata uhakika wa uvumi dhidi ya Bi Ndosi ambaye alikuwa akisingiziwa uchawi. Kutokana na ujasiri wake, Gwake Bi Ndosi aliweza kupata faraja na msaada. Hatimaye, kijiji chote kikaja kupata ukweli kuwa kumbe Bi Ndosi alikuwa akionewa tu, hakuwa mchawi kabisa. Katika *Bahati na Mumewe*, tunaona ujasiri wa Sina-Kitu ukifanikisha kumwokoa Bahati ambaye alikuwa hatarini kuliwa na mazimwi. Ujasiri wa Helena katika *Kimbia! Helena, Kimbia!* ulimwezesha kukimbia na kuokoa uhai wake huko Rwanda na Kongo. Ujasiri wa Wema katika *Wema na Albino* ulifanikisha jamii yake kupata elimu sahihi kuhusu ulemavu wa ngozi (ualbino). Pia, ujasiri wa Bure katika *Usiku wa Balaa* unamwezesha kusalimika katika vita na madhila yaliyofuata baada ya vita vile vikali kati ya Waingereza na Wajerumani. Mtu akiwa hana woga, anaweza kuthubutu kufanya mambo mengi. Pasipo woga, wasichana wanaweza kuthubutu kushindana na wavulana katika masomo yote katika shule za sekondari na kuachana na dhana potofu kuwa masomo ya sayansi ni kwa ajili ya wavulana tu. Pia, bila woga, wanawake wanaweza kushindana na wanaume katika nafasi mbalimbali za utawala au uongozi.

**Kusawiri Watoto wanaoishi katika Maisha ya Umoja**

Baadhi ya kazi za fasihi zinajaribu kuwapa watoto maadili ya kuishi kindugu katika jamii. Watu weupe na weusi na watu wenye ulemavu wa ngozi na viungo vingine wanaoneshwa kuishi kama watu wenye ubinadamu sawa wanaoishi katika amani na upendo. Wema katika *Wema na Albino*, pamoja na magumu yanayomkuta, anajaribu kutafuta njia ya kumfanya Noa ajisikie kuwa wako sawa. Wema anachukia unyanyapaa unaofanywa na wanajamii dhidi ya watu wenye ulemavu. Katika *Kijana Hodari*, tunaona kuwa, ingawa Kamau hapo awali alikuwa na uwezo mdogo kimasomo, anaweza kuishi na wenzake akina Maria na Issa wakamtia moyo na kumpenda. Kamau hajioni mpweke bali anazidi kufarijika na kupata nguvu za kuendelea kujaribu. Matokeo yake, anakuja kuwa mtu maarufu kutokana na kipaji chake. Katika *Vipaji vya Helena*, tunaona kuwa baada ya Helena kufika Uingereza na kuzoea mazingira, anapelekwa shuleni. Shule hiyo ina wanafunzi zaidi ya 500, huku akiwa Mwafrika peke yake. Ingawa mwanzoni wapo baadhi ya watoto weupe wanaoshangaa kumuona alivyo mweusi, bado anapewa upendo. Anampata Lucy ambaye anaishi naye vizuri, ingawa Lucy ni mzungu. Pengine kupitia hali hiyo, ndiyo maana Helena anapata uwezo wa kuonesha vipaji vyake. Katika *Yatima*, tunamuona Katiwa baada ya kuishi na watoto wengine, huku akiishi na babu na bibi, anaweza kuonesha uwezo wake wa kimasomo mpaka akaongoza darasa zima. Watoto wanapaswa kupewa mazingira ya

kuwawezesha kuishi kwa umoja kama Waafrika ili waweze kushirikishana mambo mbalimbali waliyonayo. Katika *Ngome ya Mianzi*, Nyawelu na Mugoha walikuwa watoto waliozaliwa wakiwa majirani, lakini wanaishi kama ndugu kabisa na kuwezesha ukombozi wa jamii yao. Nyawelu na Mugoha wanashirikiana kama kaka na dada katika mapambano ya Wadachi. Ukaribu na udugu wao ulikuwa na maana sana katika harakati za ukombozi wa jamii yao. Katika *Safari ya Muzimuni*, Sara na Chidi wanashirikiana kama ndugu kabisa wa damu moja. Kutokana na kuishi kidugu, wanaweza kupeana mawazo na kuyatekeleza ili kuleta ukombozi kwa nchi yao ya Wasifwe.

**Kuwapongeza Watoto Wanapofanya Vizuri**

Watoto hupenda kupongezwa, hasa pale wanapotimiza wajibu au kufanya vizuri katika masuala fulani, kwani hii ni hulka yao kisaikolojia. Wanaposifiwa katika mazuri wanayoyafanya, kuna uwezekano wa kuendeleza mazuri yale katika maisha ya baadaye. Wanafasihi wengi hujaribu kulizingatia hili katika kazi zao kama njia ya kuwaandaa watoto kuwa wazuri wa leo na kesho.

Ifuatayo ni mifano ya pongezi zilizotolewa kwa watoto kutoka katika vitabu teule:

> "Ninaye mtoto mmoja tu, mwenye ujasiri na upendo wa ajabu, upendo wa kuigwa na kila mtu, anaitwa Wema. Wema hebu njoo hapa watu wakuone vizuri." (*Wema na Albino*, uk. 36).

> "Wanakijiji wote walikusanyika. Mzee Pazi alianza kusema, 'Wananchi wenzangu, nimeitisha mkutano huu ili kuwashukuru waliokuja kututembelea na vijana wetu wengine kwa yote waliyoyafanya. Kwa ujasiri wao, tumeweza kugundua ujanja wa wezi waliokuwa wakiiba bidhaa za kijiji." (*Vijana Jasiri*, uk 57).

> "Baada ya maelezo hayo Bibi alisema, Wanangu usiku umewakuza. Nyinyi si watoto tena. M watu wazima" (*Moto wa Mianzi*, uk. 25).

Nukuu zote hizo zinaonesha kuwa watoto wanapenda kupongezwa. Kama tabia hii ya kupongezwa ikiendelezwa na wanajamii kupitia fasihi yao, kuna uwezekano wa kuwa na jamii inayojali na kuthamini juhudi na mchango wa kila mtu katika jamii. Katika *Tanzua*, tunamuona Gwake anavyopongezwa na Bi Ndosi kabla hajafa kutokana na ugunduzi wake. Sina-Kitu, katika *Bahati na Mumewe*, anapongezwa sana na wazazi wake baada ya kumwokoa dada yake Bahati. Katika *Kijana Hodari*, baada ya mtoto Kamau kuonesha kipaji chake cha ajabu, anapongezwa sana na walimu wake. Katika *Safari ya Muzimuni*, Sara na Chidi wanapongezwa sana baada ya kuleta ukombozi kwa nchi ya Wasifwe. Katika *Vipaji vya Helena*, tunamuona Helena akipewa zawadi na kupelekwa kwenye maonesho kutokana na kipaji chake cha ajabu cha kuchora picha za matukio mbalimbali. Hivyo, usawiri wa watoto wanaoonesha vipaji vyao na

kupongezwa, unaweza kuwajenga vizuri watoto na kuwafanya waanze kuonesha vipaji vyao kwa faida yao na jamii.

**Watoto kama Mifano Bora ya Kutoa Msamaha**

Katika jamii nyingi za ulimwengu wa leo, suala la msamaha limekuwa gumu. Familia nyingi zimesambaratika kwa sababu wazazi wamekataa kusameheana. Ndugu na ndugu waliokosana wameishi katika uhasama kwa sababu tu ya kila upande kukataa kusamehe. Katika *Safari ya Muzimuni*, tunawaona Sara na Chidi wakifanikisha suala la msamaha. Wanajamii ya Wasifwe waliokuwa wamekosa kwa kuharibu mazingira, walisamehewa kupitia vijana hawa. Kama si wao, basi nchi nzima ya Wasifwe ingeangamizwa na kutoweka kabisa. Katika *Vipaji vya Helena*, tunamuona Helena akiwa mwepesi wa kusamehe na kuukubali urafiki wa Lucy. Hapo awali, Lucy ndiye aliyekuwa anasugua ngozi ya Helena ili aone kama inatoa masizi kwa sababu tu ya weusi wa ngozi hiyo. Hata hivyo, Helena hakuwa mtu wa kinyongo, bali anamsamehe na kukubali kuwa rafiki yake. Katika riwaya ya *Yatima*, baada ya babu yake Katiwa kumsimulia jinsi alivyosababisha vifo vya wazazi wake, Katiwa anamsamehe babu bila masharti yoyote. Katika riwaya ya *Kijana Hodari*, ingawa Kamau hapo awali alikuwa akichekwa sana na rafiki zake kutokana na uwezo mdogo, anakuwa mwepesi wa kuwasamehe kabisa. Uandishi unaoonesha watoto wakiwa mifano mizuri ya kusamehe unaipa jamii mwelekeo mzuri kwa sababu ni jambo la kawaida kwa binadamu kukoseana. Kama hakuna tabia ya kusameheana, jamii inayojengwa itakuwa ya visasi na yenye hatari kwa sababu watu hawawezi kuishi pamoja kwa upendo kama hawasameheani.

**Hitimisho**

Katika makala hii, tumeeleza kuwa, kazi za fasihi zinaweza kuwaathiri watoto katika hali nzuri au mbaya. Wasomaji/wasikilizaji wa fasihi hubadilika mara baada ya kuipitia kazi ya fasihi. Mabadiliko ya wasomaji/wasikilizaji wa fasihi yanaweza kuwa chanya au hasi kutokana na kazi aliyoisoma/kuisikiliza. Wito kwa wanafasihi katika makala hii ni kulinda maslahi ya jamii, hasa katika kuandaa kazi za watoto. Kama ilivyoelezwa hapo awali, watoto wa leo ni watu wazima wa kesho na hatimaye taifa la kesho. Kama tukiathiri vibaya fikra zao leo, tutegemee kuwa na mustakabali mbaya wa jamii zetu. Lakini, kama fikra za watoto zikijengwa vizuri leo, tutarajie kuwa na jamii zenye mustakabali mzuri. Ingawa mtu anaweza kujiuliza kuwa, kama katika jamii kuna mabaya na mazuri kwa nini yote tusiyaoneshe kama yaliyo? Jibu la swali kama hilo ni kwamba, watoto bado hawajakomaa kifikra; hivyo, kwa kiasi kikubwa, watoto wanapaswa kuoneshwa zaidi mambo mazuri. Watakapokuwa wazima, wao wenyewe watakuja kuona kwa uwazi zaidi kuwa, kumbe binadamu ana pande mbili. Binadamu ni mwema pia ni mnyama hasa akiamua kujifanya kichaa. Ili kuheshimu kiwango cha fikra za mtoto, wazazi ndani ya nyumba wanapohitilafiana na kuanza kushikana

mashati, mara nyingi, hujificha chumbani ili watoto wadogo wasijue kinachoendelea. Lakini, watoto hao wakikua ndipo watakapojionea mambo barabara kwa sababu watakuwa wameshakuwa na uwezo wa kuchanganua jema na baya.

**Marejeleo**

Bakize, L.H. (2013). *Utangulizi wa fasihi ya watoto*. Dar es Salaam, Tanzania: Leonard Bakize.

Bal, M. (1997). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (2nd edition), Toronto, Canada: University of Toronto Press.

Burundi, R.N., Mukuthuria, M. & Matundura, E.S. (2014). Usimulizi katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*, *Kioo cha Lugha*, 12:73-86.

De Jong, I.J.F. (2004). Narratological theory on narrators, narratees and narratives, katika De Jong, I.J.F. na wenzake (wah.), *narrators, narratees and narratives in Ancient Greek Literature: Studies in Ancient Greek Narratives*. Leiden, Netherlands: Tuta Sub Aegide Pallas.

Dumea, P. (2009). *Usiku wa balaa*. Dar es Salaam, Tanzania: E & D Vision Publishing.

Ilomo, F. (2012). Usimulizi katika *Dunia Uwanja wa Fujo*. Tasnifu ya umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania (Haijachapishwa).

Mateso, C. (2005). *Safari ya Muzimuni*. Dar es Salaam, Tanzania: Readit Books.

Matundura, E., Kobia, J. & Mukuthuria, M. (2013). Taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto, *Mulik*a, 32: 28-47.

Memmi, A. (2006). *Decolonization and the decolonized*, translated by Roberto Bononno. London, UK: University of Minnesota Press.

Mkufya, W.E. (2008). *Wema na albino*. Dar es Salaam, Tanzania: Mangrove Publishers.

Mnyaka, O. (2005). *Kimbia Helena, kimbia!* Dar es Salaam, Tanzania: HEKO Publishers Ltd.

Mnyaka, O. (2009). *Vipaji vya Helena*. Dar es Salaam, Tanzania: HEKO Publishers Ltd.

Mulokozi, M.M. (1990). *Ngome ya Mianzi*. Dar es Salaam, Tanzania: MPB Enterprises.

Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth century literary theory***.** LIT. 224: Literature. Kampala, Uganda: Makerere University.

Mwandoloma, N. (1991). *Tanzua*. Arusha, Tanzania: Eastern Africa Publications Limited.

Mwenda, D. (1995). *Bahati na Mumewe*. Dar es Salaam, Tanzania: Education Publishers and Distributors Ltd.

Ngugi, P.M.Y. (2012). Tafsiri katika fasihi ya watoto, *Mulika*, 31: 12-26.

Ngugi, P.M.Y. (2014). Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto, *Kiswahili*, 77: 170-180.

Porini, A. (2011). *Kijana Jasiri*. Nairobi, Kenya: Vide~Muwa Publishers Limited.

Prince, G. (1982). *Narratology: The form and functioning of farrative*, Berlin, German: Mouton Publishers.

Ruthiiri, M.K. (2012). Tathmini ya ufaafu wa vitabu vya kusoma kwa madarasa ya 5 na 6 katika shule za msingi: Mifano ya waandishi wanne. Tasnifu ya shahada ya umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya (haijachapishwa).

Shija, P. (1980). *Vijana Jasiri*. Dar es Salaam, Tanzania: Tanzania Publishing House.

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*, Nairobi, Kenya: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2006). *Yatima*. Nairobi, Kenya: Vide~Muwa Publishers Limited.

Weche, M.O. (2002). Children’s literature as an image force: A case study of Ezekiel Alembi’s Books. Tasnifu ya umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya (haijachapishwa).